# Kampuni ya Israel yaanza mazungumzo ya uwekezaji sekta ya mifugo

**Na Edward Kondela**

KATIBU Mkuu Wizara ya Mifugo na Uvuvi anayeshughulikia Mifugo Prof. Elisante Ole Gabriel amekutana na kufanya mazungumzo ya awali na Mkurugenzi Mkuu wa Kampuni ya Smart Holding ya nchini Israel Avi Postelnik yenye lengo la kuwekeza hapa nchini kupitia sekta mbalimbali zikiwemo za mifugo na uvuvi.

Akizungumza juzi mara baada ya kuhitimisha mazungumzo yao ya awali katika ofisi ndogo za Wizara ya Mifugo na Uvuvi zilizopo jijini Dar es Salaam, Prof. Gabriel amesema katika mazungumzo yao wameainisha fursa kubwa zilizopo hapa nchini ikiwemo ya unenepeshaji mifugo na uongezaji thamani wa bidhaa zitokanazo na mazao ya mifugo.

Alisema nchi ya Israel ina ng'ombe ambao wana uwezo wa kutoa lita 40 hadi 50 za maziwa kwa siku moja na kwamba Postelnik amewaona ng'ombe wa aina hiyo hapa nchini katika Mkoa wa Kagera.

"Kwa bahati nzuri tayari kosaafu hiyo ya ng'ombe ameiona hapa Tanzania katika Mkoa wa Kagera na tuna dume la ng'ombe kutoka nchini Israel, ambalo lipo katika Kituo cha Taifa cha Uhimilishaji (NAIC) kilichopo Mkoani Arusha." alifafanua Prof. Gabriel.

Aidha, aliongeza kuwa mkakati mzuri ukiwekwa baina ya Tanzania na Israel katika kukuza sekta ya mifugo hapa nchini, wafugaji wanaweza kupata faida kubwa hasa baada ya Israel kuwa na teknolojia ya kutengeneza malisho ya mifugo kwa kutumia mabaki ya mazao ya mifugo.

Katika mazungumzo hayo wamegusia umuhimu wa masoko ya bidhaa za mifugo na uvuvi, ambapo wamekubaliana kuwa na masoko ya bidhaa za mifugo na uvuvi katika nchi mbalimbali kutaleta hamasa zaidi kwa wafugaji na wavuvi kuzalisha zaidi bidhaa zao.

Katika mazungumzo hayo ya awali ya Katibu Mkuu Wizara ya Mifugo na Uvuvi anayeshughulikia Mifugo Prof.Elisante Ole Gabriel na Mkurugenzi Mkuu wa Kampuni ya Smart Holding ya nchini Israel Bw. Avi Postelnik wamesema eneo ambalo wanalipa kipaumbele kwa sasa katika sekta ya mifugo ni ufugaji wa ng'ombe na uzalishaji wa mazao yatokanayo na ng'ombe ukifuatiwa na ufugaji wa kuku.



Mkurugenzi Mkuu wa Kampuni ya Smart Holding ya nchini Israel, Avi Postelnik (wa kwanza kulia) akifafanua jambo kwa Katibu Mkuu Wizara ya Mifugo na Uvuvi anayeshughulikia Mifugo, Prof. Elisante Ole Gabriel na Mkurugenzi wa Huduma za Mifugo kutoka katika wizara hiyo, Prof. Hezron Nonga, mara baada ya Postelnik kufika katika ofisi ndogo za Wizara ya Mifugo na Uvuvi zilizopo jijini Dar es Salaam, kwa ajili ya mazungumzo ya awali na katibu mkuu huyo juu ya nia ya kampuni yake kuwekeza katika sekta mbalimbali nchini zikiwemo za mifugo na uvuvi. (Picha na Edward Kondela, Afisa Habari - Wizara ya Mifugo na Uvuvi).

# Mazingira wezeshi kunufaisha Watanzania uvuvi bahari kuu

**Na Hawa Abdallah,**
ZANZIBAR

KAIMU Mkurugenzi wa Mamlaka ya Kusimamia Uvuvi wa Bahari Kuu Jamuhuri ya Muungano wa Tanzania, Emanuel Andrew, amesema kuanza kutumika sheria mpya na kanuni za kusimamia na kuendeleza uvuvi wa bahari kuu kutaongeza uwekezaji kwa wazawa.

Aliyasema hayo katika mkutano wa wadau wakiwamo wanabahari na kuongeza kuwa kanuni zake zinalenga kuchochea uwekezaji katika uchumi wa bluu hasa kwa wazawa ili kuiendeleza sekta hiyo, kwani zipo nchi nyingi zimefanikiwa kutokana na kujiendesha kwa uvuvi na utalii.

Alisema ili kufikia lengo hilo katika utungaji wa sheria, serikali imetoa vivutio kwa wazawa hasa kwa vitu ambavyo vinahitaji gharama kubwa ikiwamo vifaa vinavyoingizwa kwa ajili ya uvuvi, kupunguza ada ya leseni na vifaa vyengine.

Alibainisha kuwa wazawa wanaweza kufaidika na uvuvi wa bahari kuu iwapo sekta binafsi zitawekeza katika eneo hilo na kupata faida ikiwemo ajira, chakula na viwanda kukua.

"Wavuvi wetu wadogo hawana uwezo wa kuvua bahari kuu na badala yake maji yetu yanavuliwa na meli za nje na kusababisha Tanzania isifaidike," alibainisha.

Aidha, alisema Tanzania ilikuwa inapata chini ya asilimia 10 ya faida katika uvuvi wa bahari kuu hivyo kupitia sheria hiyo mapato ya nchi yanaweza kukua kutokana na uvuvi huo.

Alisema ni wakati wa wavuvi kutumia fursa hiyo kwa kuvua katika bahari kuu ili kufaidika na sekta hiyo kwani uchumi wa bluu una faida kubwa.

"Sekta hii ina faida nyingi ikiwamo ajira na kukuwa kwa nyororo wa thamani sasa ni wakati kwa wazawa kuitumia fursa hii," alibainisha.

Alisema Zanzibar imeshaingia mkataba ujenzi wa bandari ya uvuvi katika eneo la Mpigaduri Unguja na Mkoani kisiwani Pemba.

Akiwasilisha mada ya sheria na kanuni za mamlaka Ofisa Sheria wa Mamlaka, Keis Issa Abdallah, alisema sheria hiyo imezingatia mambo mbalimbali ikiwamo uhifadhi, usimamizi na uendelezaji wa rasilimali katika ukanda wa uchumi wa bahari ya Tanzania (EEZ).

Aidha, alisema mambo mengine ni kuongeza wigo wa mipaka ya usimamizi wa meli zenye kupeperusha bendera ya Tanzania na kuzingatia mikataba na miongozo ya kikanda na ya kimataifa ya usimamizi wa ukanda wa uchumi wa bahari na rasilimali za uvuvi zinazopatikana baharini.

Alisema kifungu cha 45 na kanuni 47 vya sheria hiyo vimetoa fursa kwa mwekezaji mzawa au kampuni ya Tanzania inayomiliki zaidi ya asilimia 51 na mzawa kuomba vivutio kupitia mamlaka.

NIPASHE UK. 17, Aprili 19, 2021

Scanned with CamScanner

i ya familia zilizoamua kuondoka eneo hilo kwa hiari

# Familia 10 za wafugaji, wakulima zapewa siku saba kuhama Bonde la Wembere

**Na TIGANYA VINCENT,** *TABORA*

FAMILIA 10 za wafugaji na wakulima, ambazo zilikuwa zimebaki katika eneo la Bonde la Wembere, Wilayani Igunga, zimepewa siku saba kuondoka kwa hiari kabla hatua za kisheria hazijachukuliwa dhidi yao.

Agizo hilo lilitolewa jana na Mkuu wa Mkoa wa Tabora, Dk. Philemon Sengati, alipofanya ziara katika Bonde la Wembere, kukagua utekelezaji wa agizo la kuwataka watu waliokuwa ndani ya bonde hilo kuondoka kwa hiari.

Alisema hadi sasa, zaidi ya familia 200, zimeondoka kwa hiari katika eneo hilo na kwenda eneo maalumu, ambalo wamepangiwa na serikali ya kijiji kwa kushirikiana na wilaya.

Famila hizo 10, zimeendelea kubaki eneo hilo, licha ya kupatiwa elimu kuhusiana na umuhimu wa hatua hiyo.

Mkuu wa mkoa, alisema katika mkutano wa hadhara, uliofanyika katika Kijiji cha Makomero, Machi, mwaka huu, walikubaliana kaya 13, kati ya 200, zilizokuwa zimebaki ndani bonde hilo, ziondoke na ziende eneo walilopangiwa, lakini ni kaya tatu, ndizo zilitekeleza agizo hilo.

Alisema familia hizo zimeendelea kubaki eneo hilo kutokana na kupotoshwa za watu wasio wema.

Kutokana na hali hiyo, Dk. Sengati, alimtaka Mkuu wa Wilaya ya Igunga, John Mwaipopo, kwa kushirikiana na polisi wilayani humo, kumtafuta kinara wa mgomo huo, ambaye ni kiongozi wa kundi la wakulima Kilimanjalo, Masandu Masaganya na wenzake wawili, ambao wamekuwa wakiwahamasisha wenzao kutoondoka.

"Hizi kaya 10 zilizobaki, ndani ya siku saba ziondoke ili serikali iweze kutekeleza majukumu yake katika eneo hili. Ndani za siku saba, sitarajii kuzikuta kaya hizi zikiwa bado zipo ndani," alisisitiza.

Aidha, mkuu huyo wa mkoa, alisema hatarajii kuona wanasiasa wanatumia siasa katika eneo hilo, ambalo lina maslahi mapana kwa maendeleo ya nchi na kuongeza kuwa, Tanzania siyo kisiwa, imeridhia mikataba mbalimbali ya kimataifa, ikiwemo kutunza na kuhifadhi maeneo oevu.

Alisema ni kinyume cha sheria, kaya hizo kuendelea kuwemo ndani ya eneo hilo, kwa kuwa ni mali ya serikali na linayo maslahi mapana ya nchi, ikiwemo utafiti wa gesi na mafuta unaoendelea, pia eneo hilo ni chujio la maji kuelekea Ziwa Eyasi.

Dk. Sengati, alitaja maslahi mengine yanayopatikana ni uwepo wa ndege aina ya flamingo, ambao wanapatikana maeneo machache duniani, pia ni njia ya wanyamapori kuelekea Pori la Akiba la Rungwa.

Mkuu huyo wa mkoa, alisema ofisi yake itafanya majadiliano na Ofisi ya Makamu wa Rais Mazingira; Wizara ya Maliasili na Utalii; Wizara ya Nishati; Wizara ya Maji na Wizara ya Ardhi na Maendeleo ya Makazi ili waweze kuainisha eneo lenye maslahi mapana ya nchi na litakalobaki wapewe wananchi kwa utaratibu mzuri.

Alisema kaya zilizobaki katika eneo hilo, zimejimilikisha maeneo makubwa, ambayo ni mali ya serikali na kuyatumia kwa maslahi binafsi, ikiwemo kuwakodisha wafugaji.

**Katika hatua nyingine,** Mkuu huyo wa mkoa, alisema wataendelea kuhakikisha maeneo yote ya hifadhi yanalindwa na kuwazuia wavamizi kuingia na kufanya uharibifu.

Mkuu wa Polisi, Wilaya ya Igunga, Ally Mkalipa, alisema Kamati ya Usalama ya Wilaya ya Igunga, ilikwenda katika eneo hilo kutathmini kaya zilizomo ndani yake, kukaa nao na kuonyeshwa eneo watakalohamia.

Alisema kaya nyingi zilionyesha kulipenda eneo hilo na baadhi ziliridhia kuondoka kwa hiari, isipokuwa familia hizo 10.

Scanned with CamScanner

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
**WIZARA YA MIFUGO NA UVUVI**

# TAARIFA KWA UMMA KUHUSU UTEUZI WA BODI YA USHAURI YA WAKALA WA ELIMU NA MAFUNZO YA UVUVI (FETA).

Kufuatia uteuzi wa **Dkt.Blandina Robert Lugendo** kuwa Mwenyekiti wa Bodi ya Ushauri ya Wakala wa Elimu na Mafunzo ya Uvuvi (FETA). Waziri Wa Mifugo na Uvuvi, **Mheshimiwa, Mashimba Mashauri Ndaki,** Kwa Mamlaka aliyonayo chini ya Sheria ya Wakala za Serikali (The executive Agencies Act) ya Mwaka 1997 Sura ya 245 ikisomwa pamoja na marejeo yake ya Mwaka 2009, na Amri ya Rais ya Kuanzisha Wakala wa Serikali (Wakala wa Elimu na Mafunzo ya Uvuvi) ya Mwaka 2011, Tangazo la Serikali Na.356/2011, amewateua wafuatao kuwa Wajumbe wa Bodi ya Ushauri ya Wakala wa Elimu na Mafunzo ya Uvuvi (FETA);

1. Profesa Zackaria Samwel Masanyiwa;
2. Dkt.Modesta Medard Ntara;
3. Bibi Prisca Jovin Ngonyani;na
4. Dkt.Robert Jeremiah Kayanda.

Uteuzi huu ni wa miaka mitatu kuanzia tarehe 29 Machi , 2021. Katibu Mkuu na Menejimenti ya Wizara ya Mifugo na Uvuvi-Sekta ya Uvuvi inawapongeza Mwenyekiti na Wajumbe kwa Uteuzi huu.

**Dkt.Rashid A.Tamatamah**
**KATIBU MKUU-UVUVI**

Scanned with CamScanner

# Wafanyabiashara waonywa kuacha kutorosha mifugo nje ya nchi

NA MWANDISHI WETU

WAFANYABIASHARA wa mifugo nchini wametakiwa kuepuka kusafirisha mifugo yao kwenda nje ya nchi bila kufuata utaratibu kwa kuwa serikali itakosa mapato kupitia rasilimali za nchi na pia ni kosa kisheria.

Akizungumza jana (14.04.2021) wakati alipotembelea eneo ambalo Wizara ya Mifugo na Uvuvi imepewa na Kijiji cha Horohoro Kijijini, kilichopo Wilaya ya Mkinga Mkoani Tanga, kwa ajili ya kuanzisha mnada wa mifugo wa mpakani, Katibu Mkuu wa wizara hiyo anayeshughulikia Mifugo Prof. Elisante Ole Gabriel amesema wizara haitakuwa tayari kumtetea mfanyabiashara yeyote atakayebainika kutenda kosa hilo.

Prof. Gabriel amesema Wizara ya Mifugo na Uvuvi imedhamiria kuanzisha mnada wa mpakani kati ya Tanzania na Kenya katika Kijiji cha Horohoro Kijijini kabla ya mwaka ujao wa fedha 2021/22 ili kudhibiti baadhi ya wafanyabiashara ambao wamekuwa wakitorosha mifugo kwenda nchi ya jirani kwa ajili ya kuuza.

"Mfanyabiashara akibainika kufanya hivyo atashughulikiwa kwa kutumia mkono wa sheria, kwani kwa kufanya hivyo inakosesha serikali mapato kupitia rasilimali za nchi." Amefafanua Prof. Gabriel

Ameongeza kuwa eneo hilo ambalo wizara imepatiwa na Kijiji cha Horohoro Kijijini lina ukubwa wa ekari 23 na lipo kando mwa barabara kuu ya kuelekea mpakani mwa Tanzania na Kenya, hivyo uwepo wa mnada huo utawezesha wafugaji wa Tanzania kuuza mifugo yao kwa wafanyabiashara wa nchi hizo mbili.

Ametoa wito kwa wafugaji Mkoa wa Tanga na mikoa ya jirani kuwa malighafi ya biashara ya minada ni mifugo, hivyo watambue jitihada za serikali na kumuunga Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mhe. Samia Suluhu Hassan ambaye ameitaka Sekta ya Mifugo kusogeza huduma zinazotakiwa kwa wafugaji ili mifugo yao isikonde na wafugaji wasikonde kiuchumi.

Amebainisha kuwa nia ya Wizara ya Mifugo na Uvuvi ni kuhakikisha Sekta ya Mifugo inachangia zaidi katika pato la taifa hivyo ni lazima kudhibiti utoroshaji wa mifugo kwenda nchi za jirani.

Kwa upande wake Mwenyekiti wa Serikali ya Kijiji cha Horohoro Kijijini Bw. Jumapili Yohana amesema wameamua kuipatia Wizara ya Mifugo na Uvuvi eneo hilo bila malipo yoyote wakiamini uwepo wa mnada mpakani katika kijiji hicho kutachangia kwa kiasi kikubwa kuongeza ajira na kukuza biashara zingine ikiwemo ya vyakula.

Yohana amesema kijiji kimefuata taratibu zote za ardhi na kukubaliana kuwa mara baada ya mnada huo utakapoanza kufanya kazi utachangia kwa kiasi kikubwa maendeleo ya kijiji chao na kushukuru wizara kwa ushirikiano.

Pia, Katibu Mkuu Wizara ya Mifugo na Uvuvi anayeshughulikia Mifugo Prof. Elisante Ole Gabriel akiwa katika ziara ya siku moja Mkoani Tanga amefika Taasisi ya Utafiti wa Mifugo nchini (TALIRI) na kujionea shughuli mbalimbali ikiwemo ya tafiti ya malisho bora ya mifugo na kuwaasa wafugaji kuipatia mifugo yao malisho bora ili iweze kuwa na afya njema na kuwa na nyama bora, maziwa bora na ngozi bora.

Amewataka wafugaji kufuga kisasa kwa kutumia sayansi na kuitaka TALIRI kusambaza tafiti zao mikoa mbalimbali ili wafugaji waweze kupata elimu ya kufuga kisasa na kuwa na mifugo bora na yenye afya ambayo itakuwa na tija kiuchumi.

Amewaasa pia wawekezaji na watu wanaofikiria kuwekeza, wafikirie kuwekeza katika malisho ya mifugo ili malisho bora yapatikane kwa wingi kwa kuwa wafugaji wengi wameanza kubadili fikra za ufugaji na kuhitaji malisho ya kisasa na kisayansi ambayo yanafaa kwa matokeo chanya ya mifugo yao.

Prof. Gabriel katika ziara yake ya siku moja Mkoani Tanga ametembelea pia Ranchi ya Mzeri iliyopo Wilaya ya Handeni na kuzungumza na wawekezaji waliopatiwa vitalu katika ranchi hiyo na Kampuni ya Ranchi za Taifa (NARCO) na kukemea tabia ya baadhi ya watu wanaoiba mifugo kwenye maeneo mbalimbali nchini ikiwemo kwenye ranchi.



*Katibu Mkuu Wizara ya Mifugo na Uvuvi anayeshughulikia Mifugo Prof. Elisante Ole Gabriel akikamua maziwa kutoka kwenye moja ya ng'ombe wanaopatikana katika Taasisi ya Utafiti wa Mifugo nchini (TALIRI) Kituo cha Tanga baada ya kufanya ziara ya kikazi ya siku moja mkoani humo na kuitaka TALIRI kusambaza tafiti zao maeneo yote nchini ili wafugaji wanufaike. (Picha na Mpiga Picha Wetu)*

Scanned with CamScanner